# NGURUMO ya MWANDISHI

Toleo La VIII-Mei-MMXXII



Hatua moja mbele...

Dawati la Mhariri:
0766-974 865

# HATUA MOJA MBELE...

**Tumeuanza mwezi Juni, napenda kukusalimuni nyote kabisa. Ni matumaini yangu mu wazima bukheri wa afya.**

Ni mara nyingine tena jarida letu linakufikia mikononi mwako. Labda ulilisubiri kwa hamu sana au ndiyo mara yako ya kwanza kulipata, yote ni sawa, hujachelewa. Jambo lamsingi tu ni kuwa ukilipata jarida hili basi mtumie na mwingine ili asome, aburudike, ajifunze na kuelimika.

Mwezi Mei umekuwa mwezi mzuri sana kwetu sote. Mimi daima hupenda sana kila ninapopata nafasi kupitia kazi mbalili za waandishi lakini zaidi kuyafuatilia Maisha yao. Ngoja nikwambie kitu rafiki, katika Maisha lazima uwe na malengo. Kama wewe huna malengo basi wewe ni maiti kwa kuwa maiti haina malengo.

Katika pitapita zangu mwezi Mei nimejifunza kitu kikubwa sana na ndicho ninapenda kuwashirikisha, labda na wewe utajifunza kitu. Kupiga hatua ni kufika mbali katika safari yako. Nimekutana na watu wanaofanya jitihada kubwa sana kwa jasho na maji ili kufikia malengo yao. Wanaoutunza na kuutumia muda vizuri kutimiza ndoto zao. Wanaotumia kile kidogo walicho nacho ili kuifanya ndoto kuwa kweli. Aisee acha kabisa. Nikajiuliza, vipi kuhusu sisi waandishi, tunapambana vipi kuweza kupiga hatua mbele?

Vijana wengi kwa sasa wameibuka kupenda kuandika riwaya na siku moja kuwa na vitabu vyao madukani lakini kila mmoja ana lengo lake. Mwingine anajisikia furaha tu kuwa mwandishi, mwingine anataka ajulikane tu kwa watu. Mwingine anataka kufanya uandishi kuwa ndiyo ajira yake, ale, anywe, avae, atunze familia kwa uandishi. Hebu jiulize wewe upo kundi gani?

Katika chunguzi zangu nimegundua kwamba wachapishaji wanaoibukia sasa ni walewale ambao ni waandishi wa riwaya kama mimi na wewe. Nikajiuliza ‘kwani wameacha uansihi?’ nilipochunguza sana nikakuta kwamba si wa meacha uandishi bali wameamua kupiga hatuaa moja mbele ili kukidhi haja ya waandishi. Ninawasifu sana akina Ibrahim Gama, Stallone Joyfull, Suleiman Kijogoo kwa kusimamia ndoto zao na kupiga hatua. Tunashuhudia kazi nzuri kabisa zikichapwa na wao.

Tumeshuhudia watu wakijinyakulia tuzo za uandishi ndani na nje ya nchi. Nikajiuliza kwani wao wanaandika nini hasa ambacho mimi na wewe hatuwezi? Nikapitia maandiko yao nikaona ni yaleyale. Nilichojifunza ni kuwa waliwekeza kwenye ndoto zao. Waliamua kupiga hatua kufika levo ya mbali hasa kimataifa. Mimi na wewe tunakwama wapi?

Ukitaka kufika safari yako lazime upige hatua. Hivyo shime waandishi tuandike katika ndoto zetu. Tupige hatua mbele kama Frank Masai kwa kutuletea ubunifu mpya wa jarida la Tulizo. Jiulize naweza nikawapa nini kipya Watanzania na wapenda fasihi! Usiangalie kwanza faida bali angalia kwanza nini cha kuwapa na faida utaiyona baadae.

Ili ufike kote huko yakupasa usome mambo mbalimbali, wasome waandishi waliotangulia na wenye mafanikio yao. Jifunze kwao, ikibidi wafuate wanunulie hata soda wakwambie  ni vipi walipenya na ni vipi walisimamia ndoto zao.

Nikutakieni mwezi June wenye mafanikio na mema mengi

**Richard Mwambe**
**04/06/2022**
**Iringa-Tanzania**

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**MHARIRI: RICHARD MWAMBE**

**MSAIDIZI: REY STANLEY**

**WASILIANA NASI**

**0766 974 865 AU 0672 160 016**

**WhatsApp: +255 734 550 514**

# MWANDISHI WETU: TATU KIONDO

Naitwa Tatu Kiondo, nimezaliwa Dar es Salaam, ninaishi Ubungo. Historia yangu katika uwanja wa fasihi ilianzia nikiw wakati nikiwa Shule ya Msingi, darasa la nne. Nilianza kuandika hadithi kwa kutumia michoro kwenye daftari kisha nawapa wanafunzi wenzangu wasome.

Nilipoingia Sekondari niliendelea kuandika ila siyo sana sababu nilijikita sana kusoma. Nilipenda sana kusoma hadithi kupitia magezeti , kuna kipindi nilikuwa nakwenda pale posta kwenye jengo la ushirika alipokua anafanya kazi baba yangu mdogo. Kila nikifika pale lazima anipe gazeti la Kiu nikawa nafuatilia hadithi. Baadae nikaingia kusoma kwenye vitabu vya waandishi Ben mtobwa, Hammie Rajabu Eric shigongo Patrick massawe na wengine wengi mpaka chombezo ya kina Ndauka nimesoma sana.

Safari yangu ya uandishi ilianzia mwaka 2013 kipindi hicho nilikua nafanya kazi kwenye kampuni ya mtu binafsi nikiwa kama secretary . Kila nilipopata muda, niliandika hadithi nikawa nazipeleka kwenye magazeti mbalimbali. Kuna siku nilipeleka pale Global Publishers, kipindi hicho ofisi zao zilikua Mwenge. Pale nilikutana na kaka Joseph Shaluwa nikamueleza shida yangu akasema nimuachie azipitie, Nilipoenda akaniambia zina makosa hivyo natakiwa kuzisahihisha na kuzipangilia upya.

Siku moja nikiwa kazini simu yangu iliingia ujumbe ulitoka kwa kaka Shaluwa akiniambia "Tatu mdogo wangu hongera sana nimeona hadithi yako kwenye gazeti la Habari leo" Nilifurahi sana nilimpigia kaka Shaluwa tukaongea kisha nikamshukuru maana nae hakuamini kama nilipeleka sehemu nyingine lakini mwisho wa siku Habari leo wakanikubali na kuzichapisha. Basi nikawa natuma hadithi kule kupitia *email* yao zikawa zinatoka.



Mpaka sasa nimefanikiwa kuchapa kitabu kimoja na mwaka huu nina mpango wa kutoa kingine.

Nina hadithi tisa ambazo nimeziandika pia uwa ninapost simulizi zangu bure kama burudani kupitia ukurasa wangu mpya wa facebook. Simulizi za Tatiana na Simulizi club Instagram.

Kitabu kinapatikana Duka la kona ya Riwaya, na posta kwa George.
Katika waandishi wanaonikosha katika uandishi wao ni Hussein Tuwa, Mzee Beka pamoja na Shaluwa.

Nawashukuru sana waandishi wenzangu wote kwani tumekua na ushirikiano kwa mambo mbalimbali. Pia ninawaomba waandishi tuzidishe mshikamano kuwasaidia waandishi wachanga. Tusahihishane penye makosa na si kuchekana.
Mwandishi mwenzio akitoa kitabu msaport kwa kununua kwani hutapungukiwa kitu kwa kusoma maandishi yake.

Mwisho naiasa jamii yangu tujenge mazoea ya kujisomea vitabu. Nunua usome, upe ubongo wako maarifa. Ukisoma riwaya utajifunza mengi ambayo hukua unayajua, jitengenezee uzoefu wa kujisomea utaondokana na msongo wa mawazo.

Mwisho kabisa shukrani kwa uongozi wa jarida la NGURUMO YA MWANDISHI Kwa kunipa nafasi hii kuweza kunisoma katika ukurasa huu. Mwenyezi mungu awabariki.

**Tatu Kiondo ni mmoja wa waandishi wa kike anayefanya vizuri sana kwenye uandishi. Soma kazi zake umjue zaidi.**


Penda kusoma vitabu

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Faida za kusoma vitabu:

- Msisimko wa Akili
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali
- Kuongeza Msamiati
- Huboresha Uwezo wa Kukumbuka
- Hukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri
- Huboresha Mtazamo na Umakini

# MANDIGA'S WELL KUIWAKILISHA NCHI



MOHAMMED HAMMIE

**Na Richard Mwambe**

Mwandishi wa fasihi nchini Mohammed Hammie ameteuliwa kugombea tuzo ya Fasihi ya Kiafrika ya James Currey kwa mwaka wa 2022.

Mohammed anakuwa Mtanzania wa kwanza kutajwa kwenye tuzo hizo toka kuanzishwa mnamo mwaka 2020, pia anakuwa Mtanzania pekee kuiwakilisha nchi yake.

Tuzo hizo ambazo hupokea kazi za Kiingereza, zinafanyika kila mwaka huku Mohammed akipenya kwenye nafasi ya kumi bora kupitia kitabu chake cha Mandiga's Well.

Waandishi wengine walioorodheshwa kugombea tuzo hiyo ni Rose Okeke (Nigeria), Sumaila Isah (Nigeria), David Ngumi (Kenya), Buntu Siwisa (South Africa), Esomnofu Ebelenna Tobenna (Nigeria), Chima Ugokwe (Nigeria), Evanson Njuki (Kenya), Abenea Ndago (Kenya), pamoja na Peter Muigai (Kenya).

Kila la heri Mohammed Hammie, tunaamini tuzo hiyo inakuja nyumbani.

## MAJI MANDIGA KOMIKI CHATIKISA KIGOMA

**Na: Mohammed Hammie**

Kitabu cha Maji Mandiga Komiki kimezinduriwa rasmi mnamo Mei 28, 2022 mkoani Kigoma. Mwandishi wa kitabu hicho Mohammed Hammie anasema hayo ni moja ya mafanikio yake makubwa toka alipoingia kwenye ulingo wa fasihi.

Kitabu hicho ambacho kimefadhiliwa na shirika la Simavi la nchini Uholanzi, kimepata baraka ya kuzinduliwa siku ya hedhi salama duniani, ambapo kwa Tanzania siku hiyo ilifanyika mkoani Kigoma, ikihuhudhuriwa na wadau mbalimbali hapa nchini, mgeni rasmi akiwa mke wa makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Mbonipaye Mpango.

Kitabu hicho kimezinduliwa siku ya hedhi salama duniani kwa kuwa kinaakisi changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa wanawake na wasichana, na pia kinawaelimisha kutambua haki zao za kibinadamu kwenye masuala ya maji.

Sote tunafahamu kuwa afya na hedhi salama ni muhimu kwa ustawi na uwezeshaji wa wanawake na wasichana duniani kote. Ili kuwa na hedhi salama, wasichana na wanawake wanahitaji upatikanaji wa huduma za maji, pamoja na usafi wa mazingira.


Wakati leo (Mei 28) dunia ikiadhimisha siku hiyo, Mohammed amezindua kitabu hiki ambacho tunaamini ni ukombozi kwa wanawake na wasichana kwa kupaza sauti ambazo hazikuwa zikisikika hapo kabla.




Mbali na kuzinduliwa, kitabu hicho cha Maji Mandiga Komiki pia kitaanza kupatikana rasmi kwenye mtandao mkubwa wa vitabu duniani wa Amazon, ambapo Mohammed anashirikiana na mashirika ya E-Mac Tanzania pamoja na Cemdo, ambayo yote yanafadhiliwa na Simavi, kuhakikisha kitabu hicho kinafikia malengo.

# Turejee kazi za Ben Mtobwa—01

**PITIO LA VITABU**



Neema B. Mtobwa

www.richardmwambe.com JAMVI la SIMULIZI

**Imeandaliwa na Neema Mtobwa**

Jambazi yupi anakufurahisha kwenye vitabu vya Joram Kiango? Neema anauliza.

Ninaowataja katika safu hii ni wale tu wanaonifurahisha mimi. Na wewe ningependa uwataje wanaokufurahisha kisha utume kwa whatsapp namba 0734550514 ili tuwaandike hapa. ***Hii ni challenge atakayeijibu atajinyakuia vocha ya 5000/=***

**1. Old Boy**

Akiwa na umri wa miaka 72 Old Boy angeweza kufikiriwa kuwa mwenye miaka kati ya arobaini na tano na hamsini tu. Hali i1iyotokana na ukakamavu, machachari na jinsi alivyojitunza kwa kutoruhusu ndevu kuishi kwenye kidevu chake kwa zaidi ya masaa ishirini na nne. Lakini si hilo lililompatia umaarufu Old Boy. Alikuwa mmoja kati ya watu wachache duniani ambao waliogopwa na kila serikali huku akiwa anapendwa na karibu kila gaidi duniani, kutokana na biashara yake ya kutatanisha.

Umeamua kuasi na kuanzisha jeshi la msituni ili kuipindua serikali, Old Boy alikuwa mtu wako. Atakuuzia silana, atakuuzia mbinu na kukupa 'wataalam' ambao watalipa mafunzo jeshi lako. Hutaki kuchukua nchi, lakini unataka kumwondoa duniani rais au mmoja wa viongozi wa juu, huna mtu anayekufaa kwa kazi hiyo wala nyenzo, Old Boy ni mtu wako. Hata serikali zisizojiamini, zilipohitaji kumwondoa duniani mmoja wa wapinzani wao anayetishia uhai wao madarakani, hiyo ilikuwa biashara ya Old Boy na ingefanyika kwa uhakika, mradi ufikie bei.

'Mzee kijana' huyo alikuwa akijivunia rekodi yake ya kufanikisha mauaji ya marais watatu duniani, wawili wakiwa wametokea Afrika, kuwaua wanamapinduzi wanne, kusababisha mapinduzi mara saba huku vikundi vinne ambavyo hadi sasa vingali porini vikimtegemea kwa silaha na utaalam.

Akiwa mwanajeshi mstaafu, ambaye alipigana katika vita kuu ya pili, na kushiriki kwa namna moja au nyingine katika vita baridi hasa baina ya KGB na CIA Old Boy alimjua karibu kila mtu aliyehitajika katika harakati zake na wapi alipo duniani. Hivyo mara nyingine ilimgharimu kuinua simu tu na kutoa maelekezo kwa mtu ambaye yuko upande wa pili wa dunia na mambo kwenda kama yalivyokusudiwa.

Hivyo, kazi mpya aliyopewa na mtu aliyejiita Marlone, ya kuwafuta duniani wagombea wanne wa urais katika nchi ndogo, isiyofahamika huko Afrika Mashariki, kwa malipo ambayo hayakuwa na mjadala aliiona kama mchezo tu. Kwanza watu wenyewe watakuwa wamesimama mbele ya hadhara, kama Masihi alivyosimama kwenye masalaba akisubiri kusulubiwa, jambo ambalo lingerahisisha sana kazi yake.

Pili alikuwa ameandaliwa silaha ya uhakika, iliyofichwa katika kitu umbile la kamera ambayo ingemwezesha kufanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa na kuondoka zake wakati watu wakiwa wamepigwa na butwaa. Kwa kawaida Old Boy hupenda kuandaa silaha zake mwenyewe, bila kumshirikisha mtu. Kwa hili alikuwa amekubali kwenda kinyume kidogo, kutokana na muda mdogo uliosalia. Lakini haikuwa kabla ya kukagua mchoro wa silaha hiyo kwa makini na kuridhika nao.

Alichokuwa akisubiri ilikuwa kukutaną, na huyo aliyetajwa kama mteja wake halisi, kwa jina King, ambaye aliambiwa kuwa baadaye angekuwa rais wa nchi hiyo, ili wafahamiane na kuwekeana mikataba kamili.

anayekufaa kwa kazi hiyo wala nyenzo, Old Boy ni mtu wako.

**2. Adrian**

Akiwa mtu ambaye hakuwahi kufanikiwa kwa lolote katika maisha yake ya awali, Adrian alikuwa ametumia robo tatu ya uhai wake kujifunza judo na kung-fu katika himaya ya baba yake, Masta, nchini Marekani, mara baada ya kuhitimu shahada yake ya kwanza katika Historia.

Adrian ni mmoja kati ya watu ambao tayari wamepoteza utaifa asilia. Wakati baba yake alikuwa na damu ya mchanganyiko baina ya Mmarekani mweusi na Mkorea mama yake yeye alikuwa kati ya Mjapani au Mfaransa.

***Itaendelea toleo lijalo***

# MAKALA: KUTOKA RASMI HADI HOLELA



Na: HUSSEIN WAMAYWA

**Miezi kadha iliyopita, nilipita pale Maktaba kuu ya Taifa kwa ajili ya kuchukua namba za vitabu almarufu ISBN. Nilipelekwa pale na kampuni ya kuchapisha vitabu ninayoifanyia kazi ya Dhahabu Publishers ambayo ilikuwa pale kuchukua nambari nyingine kwa ajili ya vitabu vingine vinanavyotarajiwa kutolewa na Dhahabu Publishers siku za usoni.**

Mazungumzo machache niliyoyafanya na mmoja wa wafanyakazi wa pale maktaba kuu yalinipa faraja kubwa, kwamba walau sasa watanzania wanaandika hasa, wanaandika kweli kweli. Kwamba kipindi cha nyuma, miaka kumi na tano hadi ishirini iliyopita, ilikuwa ni muhali kupokea vitabu japo kumi kwa mwaka kutoka kwa waandishi wa Tanzania.

Idadi ambayo kwa nyakati hizi, vitabu kumi au zaidi hupokelewa ndani ya mwezi mmoja peke yake. Ni jambo la kujivunia ati.

Labda kwa ambao hawafahamu ni kwamba Maktaba kuu ya Taifa imepewa mamlaka ya kutoa nambari zote za vitabu vinavyozalishwa nchini. Hii ina maana kila kitabu unachokiona kina namba hiyo. Maktaba kuu inapokupa namba hizo, hukutaka kuwasilisha nakala mbili za kila kitabu unachokitoa ambacho bila shaka kina namba yake. Ni hapo Maktaba inapopata uwezo wa kujua kwamba kuna vitabu vingapi vimetolewa nchini, walioviandika ni akina nani na vimechapishwa na nani pia. Hili hutokana na zile nakala mbili walizopokea ambapo wao walitangulia kutoa namba zake kwako. Kuwasilisha nakala mbili mbili za kila kazi yako kwa Maktaba kuu ya Tanzania ni takwa la kisheria. Baada ya kusema hayo, sasa nirejee katika mada yangu ya namna ninavyoiona ari ya uandishi wa vitabu hususan vya riwaya kwa sasa, nikilinganisha na siku za nyuma.

Kwamba ari ya uandishi wa vitabu inaendelea kukua kwa kasi nchini Tanzania, hilo ni dhahiri kabisa. Kwamba vitabu vingi vinavyozalishwa nchini ni vitabu vya riwaya hilo halina mjadala. Mjadala unakuja pale tunapoanza kuangalia ubora, mantiki, usanifu na usafi wa riwaya hizo. Sio siri maandishi mengi ya sasa hivi ni machafu mno, chambilecho Cuthbert Zuberi, Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania (UWAVITA)

Miaka ya nyuma labda nianzie miaka ya 1980,1990 hadi miaka ya 2000 mwishoni kutoa kitabu, kiwe cha riwaya au amsuala mengine, haikuwa kazi ndogo hata kidogo. Ndiyo, kulikuwa na makumi kwa makumi kama sio mamia ya watu waliokuwa wakiandika riwaya na vitabu vingine kila uchao.
Licha ya utaratibu wa kawaida wa kuandika kwa kalamu na karatasi, kulikuwa na kuchapa muswada kwa taipureta, kuupeleka kwa mhariri/mhakiki akaupitia, akaurejeshea ukauboresha na kuuchapa tena kisha kuuwasilisha kwa Mchapishaji. Huko ungekutana na orodha nyingine ya kutosha ya miswada kutoka kila pembe ya nchi, hapo ungepanga foleni kusubiri zamu yake ya kupitiwa, kupitishwa na kutolewa kitabu.

Mchakato ambao angalau ungechukua si chini ya miaka mitatu mpaka kukamilika na kitabu kuingia mtaani na watu kusoma. Katika muda huo, kitabu kingepita katika mikono kadha wa kadha kikichunguzwa kana kwamba kiko maabara, kabla hakijatoka pia kingepata baraka kutoka katika mamlaka anuai kuanzia zile za wadau wa Kiswahili hadi Serikalini.

Halfu kingetolewa kikiwa kimesheheni kikiwa na kila linalotakiwa kuwepo ndani yake na kikiwa hakina ukakasi pia. Pengine ni hili lililofanya kuwe na idadi ndogo ya vitabu vilivyokuwa vikichapishwa miaka hiyo.

Tofauti na sasa, maendeleo ya sayansi na teknolojia yakiwa yametamalaki, mitandao ya kijamii ikiwa imeshika hatamu hali imebadilika kweli kweli, imebadilika kwa maana ya kubadilika hasa. Wakati huu, mtu anaweza kuchapa moja kwa

moja kutoka kichwani kupitia katika kompyuta au simu yake.
Mtu huyu anaweza kwenda maktaba kuu akapewa namba na kuchapisha kitabu chake kikiwa hakijapita hata kwa mtu mmoja zaidi kwa ajili ya mapitio, uboreshaji uhariri na uhakiki. Hapa sijazungumzia utafiti na uhalisia wa kazi za fasihi.

Hata sasa, yapo maelfu ya simulizi ambazo tayari zimechapishwa kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vya habari na kuwafikia walengwa wake huku waandishi wake wakiwa sio tu hawajamaliza kuviandika visa hivyo, bali wakiwa hawajaukamilisha utunzi wake.

Hii imepelekea kuwa na wimbi kubwa la waandishi hasa wa riwaya nchini lakini kazi nyingi zikiwa zina ukakasi wa kutisha kama sio ugwadu unaochusha na kuudhi.
Kukosekana kwa taasisi imara za waandishi ambazo zingeweza kusimamia ubora na kuipeleka fasihi mbele, kulala kwa idara za serikali zenye jukumu hilo na wakati mwingine kuligeuza jukumu hilo kuwa biashara pamoja na wataalamu wetu kujiweka pembeni kutokana na ule ukweli kwamba 'fani hii hailipi' kwa pamoja kumefanya kuwa na mchafukoge wa visa na mikasa ya hadithi, riwaya na visa mikasa ambavyo havizingatii weledi, ubora vipaji na uthabiti wake.

Nadhani wakati umefika wa wahusika kama Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) na Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) kushika hatamu na kufanya ufuatiliaji wa kazi hizi. Vyama na Taasisi za Uandishi pamoja na Serikali nao washikane mkono kuhakikisha vipaji vinakuzwa lakini vinazalisha kazi bora zitakazokuwa na manufaa kwa kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

Tukifanya hivi, kwa pamoja ongezeko la uandishi wa kazi za kubuni ambalo linaendelea kukua kwa kasi litakuwa na maana kubwa zaidi. Inawezekana tutimize wajibu wetu.

---

## MTALIMBO BOOKS YAJA NA KITABU KILA MAHALI

**Na Mwandishi wetu**

KAMPUNI ya Mtalimbo Books inayojishughulisha na uchapishaji na usambazaji wa vitabu inakuja na kampeni kabambe ya kurejesha ari ya usomaji wa vitabu iitwayo KITABU KILA MAHALI – KUSOMA SIACHI NG'O!
Akizungumza na Ngurumo ya Mwandishi mapema wiki hii, Mkurugenzi wa Mtalimbo Books, Mwamwingila Peter Goima amesema kampeni hiyo ina malengo mawili, ambayo ni kurejesha ari ya jamii kusoma vitabu na hasa vitabu vya hadithi na kuhakikisha vitabu vinapatikana kila mahali kwa bei nafuu.
"Kampeni hii tutaizindua mwezi Juni mwaka huu na tutapeleka vitabu kila mahali katika masoko, viwanda, maofisi, sehemu za biashara, mashuleni, hospitalini, vituo vya basi, vituo vya polisi hadi magerezani!" Alisema Goima na kuongeza kuwa wanatarajia mpaka mwishoni mwa mwaka huu wawe wamesambaza zaidi ya vitabu *(title 60)*.
Alisema, wameamua kufanya mradi huu baada ya kufanya utafiti na kugundua kwamba uwepo wa maendeleo ya sayansi na teknolojia, harakati za utafutaji wa maisha, pamoja na mtindo wa maisha kwa pamoja vimefanya kasi ya watu kusoma vitabu ipungue na kushuka kila kukicha.
"Hii ndiyo sababu tukaanzisha kampeni hii ambayo itaendeshwa kwa watu wote lakini zaidi ni kwa watoto kwa kuwa ukijenga kizazi cha usomaji sasa, miaka michache baadae, utakuwa na taifa linalopenda kusoma vitabu zaidi," Alisema Goima.
Goima alisema wameanza kutoa bure kitabu cha mwongozo wa Mzazi kumsaidia mtoto wake kujenga tabia ya usomaji wa vitabu, tabia ambayo atakuwa nayo hadi ukubwani.
Amesema wote wanaotaka kitabu hicho watume ujumbe katika namba +255657532334 na watatumiwa kitabu kwa njia ya whatsapp, messenger, barua pepe maana kitabu hicho kiko katika nakala laini (softcopy) pekee,

# HADITHI: USIWE MUUAJI—02



Mwandishi: JANE DAVIS

**Baaa ya kufuta mahozi, Bi. Stumai alifungua kinywahe, "Yaani jamani inasikitisha sana hali ya Masanja". "Usihofu Bi. Stumai, tuombe tu Mungu yeye huwa hashindwi na jambo lolote" Aliongea mama Masanja.**

***Endelea...***

Siku moja wakiwa chumbani kwa mgonjwa walisikia sauti ya mtu akipiga hodi kwa nje. Mkewe Masanja alinyanyuka kwenda kuangalia ni nani huyo anaepiga hodi.
Mara tu alipofika nje macho yake yalipokutana na mgeni huyo mkewe, alianza kulia, hakutoa sauti alilia kilio cha kwikwi kilichosindikizwa na michirizi ya machozi mashavuni mwake.

***********

"Mbona unalia Shem? Kuna nini?"Aliuliza yule mgeni.
"Ma-Masanja" Aliongea huku kwikwi ikimbana na kushindwa kuendelea.
"Niambie Shem, usilie,nini kimempata pacha wangu, nimemtafuta sana nimeamua kusafiri kuja kumuona hapa" yule mgeni akasema. Mkewe Masanja aligeuka na kuanza kuelekea ndani huku nyuma akifuatiwa na yule mgeni.

Waliongozana hadi chumba alicholala Masanja akiwa hajiwezi. Humo walikuta Mama yake Masanja na bi Stumai wakiwa wanazungumza huku kila mmoja ameshika tama. Tofauti na watu wengine wote waliongia mule wakaishia kulia kijana yule aliingia Kwa mbwembwe akiwa na tabasamu pana usoni mwake.

Bi. Stumai alimkata jicho kali akanyanyuka kuanza kumfuata yule kijana mgeni. Alipomfikia akampiga kofi la mgongoni.

"Kijana mpuuzi wewe umetoka huko na bangi zako unakuja kumsumbua mgonjwa wetu"Aliongea bi Stumai huku akimsukuma kwa nguvu kijana yule.

"Mwache dada mwache" Aliongea mama Masanja huku akimvuta bi Stumai watoke nje ya chumba kile. Bi Stumai akiwa anatoka alimshushia matusi mazito kijana mgeni ambaye aliishia kumtazama tu na kutikisa kichwa.

"Oyaa Masanja mshikaji wangu" Aliongea yule mgeni kwa furaha akisogea kwenye kitanda. Masikini Masanja alikuwa amelala kimya.

"Mshikaji wangu amka basi tuongee pacha'ako nimetia maguu mbona wanifanyia hivyo chalii 'angu" alizidi kuongea yule kijana huku akiushika mkono wa Masanja na kugongesha Tano. Mama Masanja alirudi ndani mpaka kwa yule kijana "Samahani mwanangu kwa hiki kilichotokea" alimwambia. Kwani alijisikia vibaya sana kijana huyo kutukanwa matusi mazito na bi Stumai. Hivyo baada ya kumtoa nje jirani yake alirudi kuomba samahani, alimheshimu sana kijana huyo ambaye ni rafiki mkubwa wa mwanae Masanja.

"Usijali mama yangu, nakwenda nitakuja tena kesho" alisema kijana yule huku akifungua pazia akatoka mule chumbani.

Kijana huyo aliyeitwa Masunga alikuwa rafiki mkubwa wa Masanja ambaye walikua na kusoma pamoja hadi wote kuwa waendesha mitambo huko machimboni Mererani. Vijana hawa walifanana kwa vingi hadi kufikia watu kuwaita mapacha, na hata kwenye kuoa walioa mabinti mapacha. Masanja alimuoa Doto huku Masunga akimuoa Kulwa ndoa zao zikifungwa siku moja. Walipotezana baada ya Masanja kusafiri kuja nyumbani kwao Tabora kusalimia na ndipo alipoanza kuugua na kupelekea kuuza hadi simu, pete za ndoa ili kujitibia.

Mwili wote ulikuwa ukimuuma Masanja kila alipoguswa tu alipiga kelele za maumivu. Hakuweza kutembea, kusimama wala kukaa kitako. Kila siku alikuwa ni mtu wa kulala tu.Kula chakula hakuweza. Chakula chake kikuu kilikuwa uji, juisi na mchuzi wa mbogamboga. Walimaliza pesa nyingi wakienda huku na kule, kwa wachungaji na hospitali kubwa kubwa lakini madaktari walikosa la kusema kwani vipimo vyao havikuonesha ugonjwa wowote japo mgonjwa alikuwa hoi.

********************

Siku ya pili kijana Masunga kama alivyoahidi alifika nyumbani kwa Mama Masanja. Mkewe Masanja alifurahi sana kumuona tena pale.

# HADITHI: USIWE MUUAJI—02

"Karibu sana shem" alimkaribisha huku akimpokea begi dogo la mgongoni.
"Asante sana shem Leo nimekuja mazima, sitoondoka hadi pacha wangu asimame tena" aliongea Masunga huku akikaa pembeni ya kitanda alicholala Rafiki yake.
"Karibu sana mwanangu,ni upendo wa hali ya juu kuja kuuguza mwenzako, ubarikiwe" alisema Mama Masanja.

Kijana yule aliposalimia Mama Masanja aliitikia salamu lakini Bi Stumai hakuitikia, alikuwa kanuna huku akigeuka pembeni na kubinua midomo yake upande haswa alipoona begi la kijana huyo likipelekwa chumba cha wageni.

"Twende nje nikakuambie kitu" Bi. Stumai alimnong'oneza Mama Masanja, walinyanyuka kwa pamoja wakatoka nje kibarazani.

"Wee mama Masanja huyo kijana ndio kahamia hapa jumla?" akauliza
"Ndio tutakuwa nae hapa anamuuguza mwenzake" alijibu mama Masanja.
"Heee unamuamini kweli kijana huyo mvuta bangi!" aliongea bi Stumai akipiga makofi kisha kujishika kiunoni.

"Huyo ni rafiki mkubwa wa mwanangu hawezi kumfanyia chochote kibaya"alijibu Mama Masanja huku akimshangaa shoga yake kwa maneno anayoongea akimhisi vibaya kijana Masunga kana kwamba anamfahamu vizuri.

"Unajua kabeba nini ndani ya hilo begi lake? Shauri yako ngoja akuulie mwanao" aliongea bi Stumai akavaa viatu vyake akaanza kuondoka pale bila kumuaga Mwenyeji wake.

Huku nyuma Masunga alibaki na mgonjwa, alianza kumkagua viungo vyake haswa miguu na mikono ambavyo ngozi yake ilipauka na kusinyaa huku ikishikana sana na mifupa. Aliendelea kumkagua mikono yake akaanza kuipigapiga kidogo kuitafuta mishipa ya damu lakini haikuonekana kabisa.

"Mwanangu unalala sana cheki hadi mishipa ya damu imelala, ila siku si nyingi utakuwa sawa mwamba" aliongea Masunga akimshika rafiki yake kichwani.

Masanja alikuwa taabani japokuwa alisikia yote wanayoongea lakini hakuweza kufungua kinywa chake kuwajibu wala macho. Masunga alilitambua hilo hivyo hakuacha kumuongelesha rafiki yake huyo. Siku hiyo Masunga aliomba vipikwe viazi ulaya kwa ajili ya mgonjwa.

"Shem huyu hawezi kula viazi, mataya yamekaza tunampatia uji tu" aliongea mkewe Masanja pindi alipoambiwa aandae viazi.

"Usijali shem pacha atakula tu mimi nipo hapa, vichemshe tu" alijibu Masunga, "na maji mengi ndani ya sufuria lenye viazi " akamwambia.

"Sasa Shem chukua ukaviinjike jikoni, uviache viive hadi vilainike sana" akasema Masunga.

"Sawa Shem"
Aliitikia mke wa Masanja.
Mwanamke huyo akanyanyua sufuria lenye viazi akatoka nalo mule chumbani, akielekea jikoni kuinjika viazi hivyo.
Baada ya dakika arobaini na tano viazi hivyo tayari vilikuwa vimeiva na kulainika vya kutosha. Mke wa Masanja aliviopoa jikoni akavimimina ndani ya hotpot, akabeba na kupeleka chumbani Kwa mgonjwa.

"Shem chakula cha mgonjwa tayari" alisema mke wa Masanja akaweka *hotpot* lile mezani sambamba na bakuli pamoja na kijiko. Masunga alilisogelea *hotpot* hilo akalifungua akiangalia chakula hicho.
"Vimeiva vizuri sana shem, niletee na kijiko cha pili"

Alisema Masunga huku akianza kupakuwa viazi kiasi na mchuzi wake. Kwa kutumia kijiko akaanza kuvipondaponda viazi. Viazi hivyo ambavyo vilikuwa vimeiva sana na kuwa laini hivyo ikawa rahisi kwake kuviponda hadi kuwa mithili ya uji mzito.

"Mwanangu ni muda wa msosi sasa usiniangushe mwana"
Aliongea Masunga huku akipokea kijiko kutoka mikononi mwa mke wa Masanja. Alimnyanyua kidogo mgonjwa akamuomba shemeji yake huyo akae nyuma ya mgongo wa mgonjwa ili waweze kumpa chakula.

***Itaendelea toleo lijalo***

# MHALIFU ALIYEIUSUMBUA FBI KWA MIAKA THELATHINI—02

***Inatoka toleo lililopita...***

**Baada ya kumaliza maandalizi haya ya msingi Carl alijichimbia katika maktaba ya umma ya Philadelphia ambapo ndipo alipofanya kama ofisi yake kwani inaelezwa kuwa alikuwa na mazoea ya kutumia muda mwingi hapo akifanya 'tafiti' na angekuwa hapo kwa wiki kadhaa ili kuhitimisha mpango wake na kuandda njia ya jinsi atakavyotekeleza tukio lenyewe..**

***Endelea…***

## UTEKELEZAJI WA TUKIO

Matukio yote ambayo Carl aliyafanya alikuwa anayetekeleza mwezi Oktoba au Novemba ambapo maeneo mengi yanakuwa yapo kwenye kipindi cha kipupwe ambapo kunaambatana na baridi kali pamoja na jua kuzama mapema!

Pia matukio yake yote aliyatekeleza siku ya ijumaa na hii ndio iliyomfanya apewe jina la *'The Friday Night bank robber'*..

Uchaguzi wake wa muda wa kufanya tukio ulimpa faida kadhaa. Kwanza kipindi cha kipupwe jua linazama mapema kwa maana ya kwamba katika Masaa yale yale ambayo benki zinakuwa zinafungwa lakini katika kipindi hiki cha majira ya mwaka giza linakuwa limeanza kuingia hivyo inampa mwanya mzuri kufanya tukio. Pia kufanya tukio ijumaa ilimaanisha kuwa ndio siku nzuri kwa benki kuwa na kiwango kikubwa cha pesa taslim. Lakini pia alitumia sababu ya kisaikolojia kuwa ijumaa wafanyakazi wanakuwa waluwalu kutokana na *weekend* kuanza hivyo umakini unakuwa mdogo..



Kwahiyo alichokifanya Carl kwanza ni kupaka 'harufu' kwenye nyumba zote zilizo karibu na benki ili kuwachanganya mbwa wa polisi wakija kujaribu kutafuta alikoelekea!

Sasa, siku ambayo Carl alikuwa anafanya tukio alivaa kinyago cha kutisha usoni ambacho kilimkaa sawa sawa kabisa ili kuficha ngozi yake na pia alivaa nguo nyingi ili kuleta mwonekano kwamba ni mnene. Na alikuwa akiingia ndani ya benki akitembea kama amechuchumaa mfano wa kaa. Vitu vyote hivi alivyovifanya watu walihisi labda alikuwa na matatizo ya akili lakini hawakujua kuwa alivifanya kwa kusudi kabisa. Alivaa kinyago cha kutisha ili kuleta picha ya kuogofya na kuficha ngozi yake, pia alivaa manguo mengi ili kuficha ukubwa wa mwili wake, na alitembea kama kaa akiwa kama amechuchumaa ili kuficha urefu wake. Hii ilimsaidia sana kwani kwa miaka 30 FBI walishindwa kung'amua mtu wanayemtafuta alikuwa wa saizi gani, kimo gani au Ngozi rangi ipi?

Carl alikuwa anasubiri dakika 5 kabla benki haijafungwa ndipo alikuwa anavamia! Hii ilimpa uhakika kuwa ndani kulikuwa na wafanya kazi pekee au wateja wachache sana wamebakia.

Akishavamia benki alitoa bastola na kuamuru watu walale chini na wasimuangalie! Mashahidi wanaeleza kuwa kwa ustadi mkubwa *(labda kutokana na mazoezi ya karate)* Carl aliruka kutoka alipo mpaka kwenye droo za ma*teller* na kuweka fedha zote alizozikuta humo kisha kwa ustadi ule ule aliruka tena mpaka upande wa wateja na kuwaamuru tena kwa msisitizo wasimuangalie na kabla hawajang'amua kinachoendelea Carl alikuwa tayari keshatoka nje ya benki na kutokomea katika msitu ulio karibu.

Inaelezwa matukio yake yote aliyatekeleza ndani ya muda usiozidi da-

MHALIFU ALIYEIUSUMBUA FBI KWA MIAKA THELATHINI—02

kika mbili! Yaani chini ya dakika mbili alikuwa tayari amevamia, amekomba hela na ameshatokomea msituni.

Carl anaeleza mwenyewe kuwa akiingia ndani ya msitu alikuwa anakimbia kwa dakika kama kumi hivi mpaka mahala ambapo anakuwa ameficha baisikeli kisha anaendesha mpaka ndani ndani kabisa ya msitu kulipo na handaki lake, akifika kwenye handaki kila kitu anakiacha hapo; fedha alizoiba, kinyago, nguo, *gloves* nk. Kisha anavaa nguo nyingine za kawaida anaendesha baisikeli anaondoka! Carl anasema kuwa ataendesha baisikeli kwa muda wa kama dakika ishirini au zaidi mpaka upande wa pili wa msitu ambapo kuna barabara na hapo kunakuwa kuna gari ameegesha linamsubiri. Anaweka baisikeli ndani ya gari anaendesha kama raia wa kawaida na kuelekea nyumbani.

Carl anasema alikuwa anaacha wiki au miezi ipite mpaka habari kuhusu tukio la ujambazi zianze kufifia ndipo anarudi kwenye ule msitu na kuchukua 'hela zake'. Baada ya hapo maisha yanaendelea na anaanza 'tafiti' kwa ajili ya tukio linalofuata..

## KUKAMATWA NA MAZINGAOMBWE YA HUKUMU

Kukamatwa kwa Carl kulikuwa kwa bahati mbaya mno!
Kuna watoto walikuwa wanacheza katika msitu uliopo karibu na nyumbani kwao! Wakiwa ndani ya huo msitu waliokota *PVC tube/pipe* iliyokuwa imefichwa.

Baada ya kuifungua ndani waligundua ilikuwa na bastola na vitu vingine kadhaa vinavyotia shaka. Wale watoto wakawataarifu wazazi wao na wazazi wao wakashauri vipelekwe polisi! Baada ya vitu hivyo kupelekwa polisi, vikachunguzwa na kukakutwa ramani.

Polisi walipoifuatilia ile ramani ikawapeleka moja kwa moja kwenye handaki dogo ndani ya msitu! Kutokana na vitu vilivyokutwa ndani ya handaki hilo polisi wakapata wasiwasi kuwa inawezekana wanapambana na kesdi nyeti kuliko uwezo wao hivyo wakawataarifu FBI!

Baada ya FBI kuwasili iliwachukua saa kadhaa tu kung'amua kuwa vitu hivyo vinahusiana moja kwa moja na jambazi wanayemtafuta kwa miaka 30, *The Friday night bank robber.*

FBI walitumia alama za vidole walizozikuta kwenye lile handaki na pia walitumia jarida dogo linalohusu kituo cha mafunzo ya karate kumtafuta Carl mpaka wakampata.

Siku Carl anakamatwa alikutwa "ofisini kwake" Maktaba ya Philadelphia *Free Library* akiwa anafanya "tafiti"

Baada ya kukamatwa na kesi kufikishwa mahakamani ilikuwa ni dhahiri kuwa Carl atahukumiwa kifungo cha maisha au aghalabu miaka 115 pasipo uwezekano wa kupata msamaha kutokana na mashitaka yanayomkabili lakini mwisho wa siku Carl alikubaliana mpango na FBI kuwa awaeleze nukta kwa nukta kuhusu matukio yote 50 aliyoyafanya, pia akubali kushirikiana na FBI kutengeneza programu maalum kuwasaidia maafisa wa FBI kutambua namna ya kuwabaini 'majambazi sugu', na pia awaelekeze kuhusu saikolojia ya kupanga matukio ya uhalifu wa hali ya juu.

Carl akakubaliana na masharti yote haya na mahakama ikapunguza adhabu yake kutoka kifungo cha maisha mpaka kifungo cha miaka 17 bila msamaha.

Hivyo basi ikifika (kadiri ilivyotafsiriwa Makala hii) 2021 Carl Gugasian anarudi uraiani! Inaelezwa kuwa huko gerezani Carl ni mtu mnyoofu mno na ni mfungwa wa kuigwa na ameendeleza desturi yake ya kupenda mazoezi hivyo yuko katika afya njema sana na wengi wanaamini atafika 2021 akiwa salama salimini na naamini kabisa Hollywood wanaomba usiku na mchana atoke salama ili watengeneze filam kumhusu.

**MWISHO**

***Imeandaliwa kwa msaada wa mtandao na kutafsiriwa na Richard Mwambe***

***Toleo lijalo tutaangazia Makala nyingine***

***0672160016***

# MPIGA MBIO — 08

*Ilipoishia*

**“Nimefurahi leo kuwa pamoja na kitinda mimba!” akamtania. Ikunda akatoa tabasamu la siri lakini Kenneth aliliona na kulipokea.**

**“Niambie basi mi nataka kuwahi…” Ikunda akamwambja Kenneth.**

***Endelea***

“Unawahi wapi! Unanyonyesha?”
“Usiku, mi’ naogopa vibaka…”
“Usijali, utapelekwa mpaka nyumbani unakoishi…”
“We! We! We! Siendi na mwanaume nyumbani kwangu…” Ikunda alijikuta anainua uso wake na kumtazama Kenny.
“Unaogopa nini umeshakuwa mkubwa sasa unahitaji kuwa na wako, au ndiye unayemwogopa?”
“Dah! Kama kuna kitu nakiogopa ni kujenga mahusiano na mwanaume…”. Maneno haya yakawa kama nyundo kichwani kwa Kenneth.
“Bibiye ….”
“Usiniite hivyo bwana, jina langu Ikunda!”
“Sawa! Ikunda… unataka kunambia hujawahi kuwa na mpenzi umri huo?” akamtupia swali. Wakiwa katika mazungumzo hayo, mhudumu aliwafikia na kuchukua oda za chakula. Alipokwishaondoka wakaendelea.

“Sijawahi…. Najua huwezi amini, lakini sijawahi,” akamjibu. Kenneth akalipokea moyoni mwake, akameza mate na kumtazama kwa makini binti huyo. Ikunda alikuwa mwanamke mwenye uanamke wake. Mfupi wa kimo, mwenye uso wa duara, mwili wake ulikuwa habari nyingine, alikatika kikike haswa. Akikupitia mbele yako lazima uhisi kiu.

Mazungumzo ya wawili hawa yalipamba moto. Saa zikapita hata Ikunda akasahau kama alisema anataka kuwahi nyumbani. Alipoitzama saa katika simu yake ilikwishatimu saa nne usiku.

“We unakaa wapi?” Ikunda aliuliza mara tu mhudumu alipoondoa vyombo mezani.
“Ununio! Karibu kabisa na fukwe, ukitaka kuogelea haya, ukitaka kuosha vyombo wewe tu…”
“Napenda sana kuogelea…” Ikunda akamwambia Kenneth. Mara hii woga ulikuwa umemwisha. Maneno matamu ya Kenneth yalimpa amani na uaminifu wa wema wa mtu huyo.
“Nakukàribisha weekend nyumbani kwangu…” akamwambia Ikunda wakati wakitaka kuagana.

“Nitaangalia!”
“Nitafurahi ukifika Ikunda…”
“Asante!” Ikunda alijikuta akitazamana usoni na kijana huyo. Macho yao yalizungumza kitu. Kitu kilichojificha ndani ya moyo wa kila mmoja kinachoweza kutolewa nje kwa kinywa au macho tu. Almanusura midomo yao ikutane kama si simu ya Kenneth kuita. Kijana huyo akiwa kamshika mkono Ikunda wakitoka nje ya mgahawa ule, aliendelea kuongea na simu. “Wapi?… palepale pa siku ile?…. Sawa! Dakika chache tu.” akakata simu na kuirudisha mfukoni. Tayari walikuwa nje kwenye maegesho ya magari.

“Ulikuwa unaongea na nani?” Ikunda akamuuliza.
“Marafiki tu, inabidi niende Ilala kuonana nao…” Kenneth akamjibu. Lakini aling'amua kuwa hali ya mwanamke huyo imebadilika. “Vipi kwan!?” akauliza.
“Mh! Wanaume!”
“Anh anh nenda tu kwa hao uwapendao…” Ikunda alibadilika, jahazi la wivu na inda likambeba. Kwa muda huo mchache aliona tayari Kenneth ni wake.



Richard Mwambe

“Ikunda, umeshahisi naenda kwa wanawake au?”
“Mi sijasema!”
“Twende basi ukawaone wanaoniita kama unafikiri nina tabia hizo…” Kenneth alimwambia kwa upole. Ikunda alisimama kimya huku mikono yake ikiwa imefumbatwa kifuani.
“Bibiye… ” akamwita huku akimshika mkono.
“Nimekwambia usiniite bibiye…”
“Oh Ikunda mpenzi!” akamshika mkono mmoja alioutoa pale kifuani, “fuatana nami kama hutojali, najua huamini… twende pamoja…” Ikunda alijikuta anamfuata Kenneth. Akapakiwa garini, siti ya mbele ndani ya Toyota Crown. “Kiti hiki kilikuwa kwa ajili yako…” akamwambia huku akiliondoa gari katika maegesho. Safari kuelekea Ilala ikaanza huku Ikunda akiwa kimya.

# MPIGA MBIO — 08



***** *****

Kenneth aliegesha gari lake nje ya kilabu cha wazee, Ilala. Hakuteremka, alibaki palepale kwenye usukani huku gari lake likiwa limewasha taa za hatari. Haikupita sekunde kumi, kioo cha upande wake kikagongwa. Akabonya mahali kikateremka taratibu na kumwona huyo aliyegonga.

"Vipi Kebby?" akamsabahi namna hiyo. Kebby, aliyekuwa amesimama upande wake nje, hakujibu haraka. Kenneth alielewa kwa nini, alimwelewa rafiki yake huyu.
"Poa mkuu, vipi wewe?" akaitikia. Kiasili Kebby alikuwa mwongeaji sana lakini awapo na jambo lililomkera huwa anakosa maneno ya kuongea mpaka ayatafute.
"Mi niko poa…"
"Vipi, ndo shemeji?" akauliza.

"We unaonaje?" Kenneth hakutaka kujibu moja kwa moja alikwepa isije kuwa mwanamke huyo bado hajajitoa kwake. Chezea kushushuliwa weye!
"Hii ndiyo shida yako Kenny… huwezi kujibu moja kwa moja, lazima na we uulize swali… unakuwa kama Yesu bwana!" Kebby akalalama.
"Kebby rafiki yangu, usikalili aina moja ya kujibu maswali, mahakamani utafungwa. Kuna njia tatu za kujibu maswali; swali kwa swali, swali kwa jibu au swali kwa maelezo…"
"Hahahahaaaaa! " Kebby akacheka,
"Za saa hizi bibiye!" akamsabahi Ikunda. Ikunda akaguna kwanza kabla hajajibu. "Salama shem vipi?"
"Safi tu!" Kebby akamjibu Ikunda, hakuwa anamwona vizuri kutokana na giza lililokuwa ndani ya gari hilo.
"Tuongee kidogo!" Kebby akamwambi rafikiye. Kenneth akamgeukia Ikunda "naomba niongee na jamaa yangu kidogo…".
"Sawa!" Ikunda akajibu. Kenneth akatoka nje na kuufunga mlango wa gari nyuma yake. Hatua kama ishirini hivi, wakasimama. Kebby akabaki kimya kwanza. Kenneth alijua kwanini, akasubiri la kusubiri.
"Sasa rafiki yangu, ndo unafanya nini?" Kebby akamuuliza rafikiye.
"We acha tu, kaning'ang'ania… ulivyopiga simu akajua nakuja kukutana na wanawake…"
"Kiongoziiiii…. Tulishakubaliana tangu awali… hivi viumbe tusivikaribishe mezani vitaharibu chakula…" Kebby akalalamika.
"Usijali, imetokea accidentally tu, si unajua hata wewe umenipigia bila miadi…"
"Ila mtoto anaonekana mkali!" Kebby akasifia.
"Ole wako!"
Kenneth na Kebby walikuwa marafiki wa muda mrefu. Walikutana kwenye moja ya vipindi vigumu vya maisha yao. Kundi lao walikuwa watatu, marafiki walioshibana, wa kufa na kuzikana. Siku hii kwao haikuwa ya kukutana bali Kebby alikuwa na jambo lake.

"Vipi imetema?" Kebby akauliza.
"Tayari mwanangu… sasa ni mpango wa kuitoa tu…" Kenneth akamwambia rafiki yake.
"Sasa Scogon yupo Kinondoni Stereo, anasubiri jibu…" Kebby akasema.
"Na yule anapapenda pale, sijui pana nini!"
"Pana nini! Hujui? Yule si kama wewe tu" Kebby akamwambia Kenneth huku mkono wake ukiwa kama anayeomba kitu na sura yake ikielekea upande wa pili. Kenneth akatoa kiburungutu cha pesa. Akatwaa vipande viwili na kumpatia.
"Kimoja chako kingine cha Scogon!"

"Mi ndo maana nakuelewa kiongozi…" Kebby akapokea zile pesa na kuzisunda mfukoni.
"Viwanja wapi?"
"Sinza!" Kebby akajibu.
"Una usafiri?"
"Kama kawaida…". Wawili hao wakaagana na kila mtu akashika hamsini zake.

***Itaendelea toleo lijalo...***

**TANGAZO:**

**Kitabu cha MPIGAMBIO kipo mbioni kutoka. Kama unahitaji kupata nakala yako, wasiliana nasi kwa namba 0672160016 au tuandikie WhatsApp 0734550514 ukamate nakala yako.**

**Ni shilingi ELFU KUMI (10000/=) TU**

## Tangazo

**NJOO TUANDAE PAMOJA TAMASHA LA FASIHI YA KISWAHILI 2022**

Taasisi Tanzania Fasihi Fund (TAFF) yenye makao yake Makuu Kisarawe mkoani Pwani inakaribisha maombi ya watu wanaotaka kujitolea kushiriki maandalizi ya Tamasha la pili la Fasihi ya Kiswahili litakalofanyika Novemba 19 na 20 katika Wilaya ya Kisawawe Mkoani Pwani.
A: **SIFA ZA MWOMBAJI:** Awe mkazi wa Tanzania katika maeneo ya mkoa wa Pwani katika Wilaya ya kisarawe ama Kibaha au Dar es Salaam.

**Elimu:** Kuanzia kidato cha sita na kuendelea, aweze kuzungumza lugha ya Kiswahili kiingereza kwa ufasaha, pia aweze kuandika taarifa kwa lugha zote mbili. Akiwa mtunzi wa Fasihi atapewa kipaumbele zaidi

**Fani: Uratibu wa programu, Mawasilino na Tehama, Ufuatiliaji na Tathmini**

**Umri:** 20-35

**Jinsia:** ME/KE

**B: AINA YA KAZI NA ENEO LA KAZI**

Kuandaa tamasha la pili la fasihi la mwaka 2022 katika Wilaya ya Kisarawe – Mkoa wa Pwani.
Kuandaa ugawaji wa tuzo za waandishi chipukizi katika Wilaya ya Kisarawe
Kuandaa taarifa za matukio hayo mawili (tajwa hapo juu)
Mtandaoni, ofisi za Taff Kisarawe
Kutembelea wadau mbali mbali maeneo ya Kisarawe, Mkoa wa Pwani na Dar es salaam.

**C: MUDA WA KUJITOLEA**

Kati ya June na Novemba 2022
Siku mbili kwa wiki
Masaa 2-6 kwa siku
Siku za wiki

**D: UTAMBUZI NA FURSA BAADA YA MRADI**

Cheti cha utambuzi kitatolewa.
Kuunganishwa katika fursa mbalimbali ziliopo TAFF
Udhamini katika ajira atakazoomba volunteer baada ya program ya TAFF ndani ya mwaka mmoja.
Nafasi ya ajira katika miradi ya TAFF pale inapotokea na kuwa ndani ya uwezo.
Fursa ya mafunzo ya kazi za fasihi

**Tuma maombi yako kwa Barua pepe: fasihifund@gmail.com au S.L.P 28120 Kisarawe, Pwani – Tanzania. Unaweza pia kupiga simu namba +255 629 139 317, 0755 697335.**

**Kumbuka FASIHI NI TUNU NA URITHI WETU**

---